



Ukweli:

Kuhusu Mpango wa Udhibiti wa Wafanyakazi wa Huduma za Walemavu

Mpango wa Udhibiti wa Wafanyakazi wa Huduma za Walemavu ulianza tarehe 1 Julai 2020.

Unajumuisha:

- Kanuni ya Maadili kwa wafanyakazi wote wa huduma za walemavu katika Victoria
- masharti ya lazima ya arifa kwa watoa huduma na wafanyakazi kutoa ripoti ya wasiwasi kwamba mfanyakazi mlemau anaweza kuwa anahatarisha usalama
- huduma ya malalamiko huru ambapo wasiwasi wa ubora na usalama kuhusu mfanyakazi yeyote wa huduma za walemavu wa Victoria anaweza kuripotiwa.

Kuhusu Kanuni

Kanuni ya Maadili ni zana muhimu ya kuwalinda watu walio na ulemavu kutokana na madhara na dhuluma kwa kutambua majukumu ambayo wafanyakazi wa huduma za walemavu wa Victoria ambao hawajasajiliwa lazima watii. Kanuni ya Maadili itatumika kwa wafanyakazi wote wa huduma za walemavu, bila kujali kama wamefadhliliwa kuitia NDIS au watoa huduma wengine.

Kanuni ya Maadili ya Ulinzi wa Huduma za Walemavu (Kanuni) imebainishwa katika Kanuni za Ulinzi wa Huduma za Walemavu 2020, ambazo ni sheria zilizowekwa chini ya *Sheria ya Ulinzi wa Huduma za Walemavu 2018*.

Kanuni hii inabainisha majukumu ambayo wafanyakazi wa huduma za walemavu wa Victoria lazima watii na inatoa kiwango cha kulinda watu walio na ulemavu dhidi ya madhara na dhuluma.

Kanuni hii imeundwa kukamilishana na Mfumo wa Ulinzi na Ubora wa NDIS ili kukuza wafanyakazi wa huduma za walemavu walio na usalama na ujuzi katika Victoria. Kanuni inatumia Kanuni ya Maadili ya NDIS, inayokuza uthabiti katika masharti ya mwenendo wa wafanyakazi katika Victoria, bila kujali kama wamefadhliliwa kuitia NDIS au watoa huduma wengine.

Kanuni za Maadili inatumika kwa nani?

Kanuni hii inatumika kwa wafanyakazi wote wa huduma za walemavu walioajiriwa au wanaohusika vinginevyo kutoa huduma za ulemavu katika Victoria, bila kujali chanzo chao cha ufadhili.

Kuhusu arifa

Mtu yeyote anaweza kutujulisha kuhusu wasiwasi pale ambapo mfanyakazi wa huduma za walemavu anaweza kuwa anahatarisha usalama. Hii inaitwa 'arifa'. Chini ya *Sheria ya Ulinzi wa Huduma za Walemavu 2018*, wafanyakazi wa huduma za walemavu na waajiri lazima wajulishe Tume ya Wafanyakazi wa Huduma za Walemavu ya Victoria ikiwa wanaamini kuwa mfanyakazi amehusika katika aina nyingine za utovu wa nidhamu.

Sehemu hii ya Mpango wa Udhibiti wa Wafanyakazi wa Huduma za Walemavu husaidia Tume ya Wafanyakazi wa Huduma za Walemavu ya Victoria ijue hatari zinazoweza kutokea kwa watumiaji wa huduma za walemavu, kwa njia hii tunaweza kuzuia na kulinda watu walio na ulemavu kutokana na madhara. Arifa inapaswa kutolewa wakati mfanyakazi wa huduma za walemavu au mwajiri anaamini kwa busara kwamba mfanyakazi wa huduma za walemavu amehusika katika mwenendo unaopaswa kuripotiwa.

Saidia kujenga sekta ya walemavu yenye nguvu na salama



Tume ya Wafanyakazi wa Huduma za Walemavu sasa inachukua malalamiko kuhusu wafanyakazi wa huduma za walemavu katika Victoria

Huduma yetu ya malalamiko ni huru, haina upendeleo na ya bila malipo. Katika kushughulikia malalamiko kuhusu wafanyakazi wa huduma za walemavu, tunakusudia kukuza ubora, usalama, mwitikio na uendelevu wa wafanyakazi wa huduma za walemavu.

Usajili wa wafanyakazi wa kujitolea wa huduma za walemavu unaanza tarehe 1 Julai 2021

Tunafahamu kuwa janga la COVID-19 linaathiri wafanyakazi wa huduma za walemavu kwa njia tofauti na linasababisha mafadhaiko na kutokuwa na uhakika katika sekta hii. Hatua ya kuchelewesha usajili kwa miezi 12 itaruhusu muda kwa wafanyakazi kurejelea ukawaida baada ya mgogoro kabla ya kujihuisha na mpango mpya wa usajili.

Kuhusu Tume ya Wafanyakazi wa Huduma za Walemavu ya Victoria

Tume ya Wafanyakazi wa Huduma za Walemavu ni shirika jipya huru. Ikiiongozwa na Kamishna Dan Stubbs, kazi yake ni kulinda zaidi watu walio na ulemavu na kujenga sekta ya walemavu yenye nguvu na salama.

Inawajibikia kanuni ya maadili, kubainisha matarajio ya chini zaidi kwa wafanyakazi wote wanaosaidia watu wenyewe ulemavu, na huduma ya malalamiko. Inapoarifiwa, ina uwezo wa kuchunguza na kupiga marufuku wafanyakazi ambao wanahatarisha usalama wa watu.

Tembelea tovuti yetu vdwc.vic.gov.au au upige simu 1800 497 132

Jisajili kwa [jarida letu](#)

Tufuate



vdwc.vic.gov.au

Piga Simu 1800 497 132